

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAISI
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA

SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO
S.L.P 65. KIMAMBA-KILOSA
TAREHE.....

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI
.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO ILIYOPO WILAYA YA
KILOSA MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari Parakuyo ipo umbali wa km 63 kutoka Morogoro mjini, kando ya barabara kuelekea Kilosa, kata ya Parakuyo karibu na stesheni ya Mkata. Usafiri ni wa basi toka Morogoro mjini, unapatikana kituo cha mabasi MSAMVU na nauli ni Tshs 6000/=. Shule hii ni ya Bweni mchanganyiko wasichana na wavulana. Ipo eneo la kijiji cha PARAKUYO kati ya Kimamba na stesheni ya Mkata Wilaya ya Kilosa.

Muhula wa masomo unanza tarehe hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe Na mwisho wa kuripoti ni tarehe Wanafunzi wanatakiwa kufika shuleni kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:30 jioni.

Mara baada ya kufika shuleni mwanafunzi atapokelewa na Mwalimu wa zamu na kusajiliwa katika Ofisi ya Makamu wa Mkuu wa shule. Mwanafunzi atasajiliwa baada ya kuwa amekamilisha maagizo yaliyotajwa katika fomu hii.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE YA SHULE

2.1.1 WAVULANA:

- i. Mashati mawili 2 nyeupe ya tetroni mikono mifupi.
- ii. Viatu pea 2 vya ngozi nyeusi na vya kamba na soksi pea 2 nyeupe zisizo na mistari au pambo lolote.
- iii. Suruali 2 rangi ya kijani iliyofifia rinda mbili isiyo bana (isiwe na mshono wa kubana)
- iv. sweta rangi ya kijivu kujikinga na baridi.
- v. T-Shirt rangi ya njano au bluu, bukta au kaptula ya rangi ya bluu pamoja na raba rangi ya bluu/nyeusi kwa ajili ya michezo au kazi za nje.
- vi. Mkanda mweusi wa ngozi
- vii. Track suti blue au nyeusi (2) yenye mistari mweupe pembeni
- viii. Vesti nyeupe (2), tochi na saa ya mkononi
- ix. Jezi za michezo nyekundu au njano iwe bukta na t-shirt yake.
- x. Blanket (1) rangi yeyote

2.1.2 WASICHANA

- i. Mashati mawili (2) meupe ya Tetroni mikono mifupi; au Hijabu - nusu kanzu nyeupe (kwa waislamu wanaohitaji).
- ii. Viatu pea (2) ngozi nyeusi na vya kamba na soksi jozi 2 nyeupe zisizo na mistari au pambo lolote.
- iii. Sketi 2 rangi ya kijani rinda boksi iliyofifia,
- iv. Nguo za michezo: T-Shirt rangi ya njano au bluu, sketi rangi ya bluu na raba rangi ya bluu au nyeusi. (na hijabu nyeusi (kwa muislamu anayehitaji)).
- v. sweta moja, rangi ya kijivu kujikinga na baridi.
- vi. Track suti blue au nyeusi (2) yenye mistari meupe pembeni
- vii. Vest nyeupe (2), tochi na saa ya mkononi
- viii. Jezi za michezo nyekundu au njano iwe bukta na t-shirt yake.
- ix. Blanket (1) rangi yeyote
- x. Majuba mawili meusi ya shamba dress kwa muislamu

2.2 VIFAA VYA CHAKULA

Awe na (i) bakuli, (ii) sahani, (iii) kikombe (iv) kijiko

2.3 MALAZI.

Mwanafunzi alete:

- i) Shuka mbili (2) rangi ya bluu kwa wavulana, rangi ya njano kwa wasichana.
- ii) Chandarua (futi 4), taulo na mto na foronya zake (2) mbili.
- iii) Godoro **futi mbili na nusu kwa futi sita (inchi imara)**
- iv) **Pazia** rangi ya njano wasichana na blue wavulana
- v) **Ndala za kuogea**
- vi) Ndoo mbili za lita 10
- vii) Sanduku la chuma na kufuli yake kwa ajili ya kuhifadhiya vitu
- viii) Sabuni za kuogea na kufulia
- ix) Mswaki na dawa ya mswaki.

2.4 MAHITAJI YA DARASANI.

1. Daftari kubwa 12 (Counter book) za kuanzia. (Quire 3)
2. Mathematical set (mkebe), Rula, kalamu ya wino (bluu/nyeusi), penseli, kifutio na begi dogo la kubebea daftari.
3. Kamusi (Dictionary) ya Kiingereza- Kiswahili

2.5 MAHITAJI MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI.

- i. Cheti cha kuzaliwa.
- ii. Bima ya afya kwa ajili ya matibabu
- iii. Nauli ya kurudi nyumbani na poket money (hela ya matumizi)
- iv. Fomu ya kupima afya (medical examination) iliyojazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali. (imeambatanishwa nyuma)
- v. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai (imeambatanishwa nyuma)
- vi. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.(imeambatanishwa nyuma)
- vii. Picha (passport size 4)
- viii. Fagio moja la chelewa kwa ajili ya usafi.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria Na 25 Ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu inchini na ofisi ya Raisi TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji wa elimu .

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

3.1 KANUNI ZA JUMLA

- (i) Yampasa kila mwanafunzi kuwepo mahali atakiwapo kwa wakati na afanye lile linalompasa kwa usahihi na ukamilifu akijua kuwa kufanya hivyo ni wajibu wake.
- (ii) Yampasa kila mwanafunzi kujua, kijiheshimu kuzilinda haki zake na wenzake kwa mujibu na kanuni/ sheria za shule.

3.2 VAZI RASMI (SARE YA SHULE)

Vazi rasmi (sare ya shule) kama ilivyoainishwa kwa wavulana na wasichana itavaliwa wakati wote wa:

- i. Masomo darasani na muda wote mwanafunzi anapokuwa shuleni.
- ii. Mhadhara (Baraza la shule).
- iii. Kutoka nje ya shule kwa shughuli maalumu za kishule au mwanafunzi anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalum.

Vitu vingine kama kofia, heleni, bangili, mikanda mipana, rangi za kucha na midomo, nywele za bandia, mikufu , mikufu ya kila aina, hilizi, rozali, kandambili, viatu vya magurudumu, nguo zilizochanika au kubana au nguo fupi haziruhusiwi kuvaliwa hapa shuleni.

3.3 MIPAKA YA SHULE

- (i) Wanafunzi hawaruhusiwi kuwa nje ya shule wakati wa masomo bila kibali maalumu kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi.
- (ii) Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kukaa au kupumzika au kufanya lolote katika eneo la majani au barabara.
- (iii) Ni marufuku wanafunzi kuonekana maeneo ya nyumba za walimu au wafanyakazi wasio walimu bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa zamu/ mlezi.
- (iv) Mwanafunzi haruhusiwi kuingia katika chumba cha walimu (Staff room) ofisi za shule au maabara bila kibali / ruhusa toka kwa mwalimu au mhudumu wa ofisi husika.
- (v) Hairuhusiwi kutupa takataka kwenye bustani za maua au viwanja vya shule. Mashimo na madebe ya kuhifadhia takataka yatumike ipasavyo.

3.4 MALI YA UMMA

Kifaa chochote cha shule ni mali ya umma (serikali). Atakayeharibu, kupoteza au kuiba atalipa fidia. Iwapo wanafunzi wengi watahusika itabidi wote walipe fidia kila mmoja kwa nafasi yake. Mwanafunzi haruhusiwi kuandika katika vitabu vya shule, kuta, madawati, viti, meza, vitanda au ubao wa kufundishia.

3.5 KUTEMBELEA WANAFUNZI

- i. Mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaweza kumtembelea mwanafunzi kwa sababu maalumu hapa shuleni siku za Jumatano(kuanzia saa 9:30 alasiri hadi saa 11:30 jioni), Jumamosi na Jumapili na siku za sikukuu (kuanzia saa 6:30 mchana hadi saa 11:30 jioni).

- ii. Mwanafunzi hataruhusiwa kuonana na mgeni yeyote wakati wa masomo au muda tofauti na ilivyoainishwa.
- iii. Mzazi/mlezi mara tu baada ya kufika shuleni ataonana na mwalimu wa zamu ambapo atamuhudumia kwa niaba ya mkuu wa shule na kumruhusu kuonana na mwanafunzi. Hairuhusiwi kabisa kumpatia mwanafunzi vitu visivyoruhusiwa shuleni.

3.6 MAWASILIANO

- i. Mawasiliano yoyote baina ya mzazi na mwanafunzi kwa njia yoyote yafanyike kupitia kwa mwalimu wa mawasiliano au mwalimu yeyote aliyeainishwa na uongozi wa shule. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kuwasiliana na mzazi au mlezi kupitia mtu mwingine tofauti na mwalimu wa shule hii.
- ii. Barua zote zielekezwe kwa mkuu wa shule.
- iii. Lugha ya mawasiliano shuleni ni kiingereza na Kiswahili tu. Marufuku kuongea lugha za kikabila shuleni.

3.7 MAHUDHURIO

- i. Wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria shughuli zote za shule kama ratiba ya shule ilivyoainisha. Uvivu haukubaliki hapa shuleni.
- ii. Ni wajibu kila mwanafunzi atii wito wa kengele na kuhudhuria roll-call zote.
- iii. Baada ya likizo wanafunzi wanatakiwa kufika shuleni tarehe iliyopangwa. Kinyume na hili watarudishwa.
- iv. Utoro shuleni ni mwiko. Mwanafunzi asipohudhuria vipindi 21 mfurulizo bila taarifa atasimamishwa masomo. Asipohudhuria miezi 3 mfurulizo bila sababu atakuwa amejifuta shule moja kwa moja.

3.8 HESHIMA

- i. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na heshima na mwenendo mzuri awapo shuleni na nje ya mipaka ya shule.
- ii. Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu/wazazi/wafanyakazi wasio walimu au mgeni yeyote anayepita karibu naye au wanapoingia darasani.
- iii. Wanafunzi wanatakiwa kutii na kuwaheshimu walimu, wafanyakazi na viongozi. Kinyume na hivyo hatua za kinidhamu zitachululiwa.
- iv. Wanafunzi wote wasimame na washiriki kuimba wimbo wa taifa mbele ya bendera ya taifa.
- v. Ni marufuku kutumia lugha za matusi, zisizorasmi (**makabila**) shuleni, nje ya shule na uwanjani wakati wa michezo.
- vi. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu na kukubali tofauti za kidini, kisiasa na kiutamaduni zilizopo katika jamii. Ni marufuku kusababisha hofu, vurugu na kuvunja kanuni za shule kwa kusingizia imani za kidini, ushirikina, siasa na mira au utamaduni. Hatua kali zitachukuliwa.

3.9 AFYA

- i. Mwanafunzi yeyote mwenye ugonjwa wowote atoe taarifa **mara moja** kwa mwalimu wa zamu au malezi.
- ii. Wanafunzi wote wanatakiwa kunywa maji yaliyochemshwa na kuifadhiwa kwenye chombo kilichosafishwa.
- iii. Ni marufuku kujisaidia nje ya choo au kutupa taka ovyo.
- iv. Wanafunzi wote watatakiwa wale chakula cha shule tu. Ni marufuku mwanafunzi kula chakula kisichopikwa shuleni. Pia hairuhusiwi kuingiza chakula darasani au bwenini. Ni marufuku mwanafunzi kuingia jikoni kujipikia au kupakua chakula mwenyewe.
- v. Mazingira ya shule ni lazima yawe safi muda wote. Kila mwanafunzi ana jukumu la kufanya usafi wa mazingira na wa kwake binafsi.

- vi. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kudumu ya kiafya atatakiwa kuleta uthibitisho kutoka kwa daktari na kuwasilisha kwa makamu mkuu wa shule. Aidha kila mwanafunzi anatakiwa kujaza fomu ya afya iliyoambatanishwa na maelezo haya kabla ya kuja shule.

3.10 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE.

Mambo yafuatayo hayatakiwi na adabu yake ni kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule moja kwa moja:

- i) Wizi
- ii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama uvutaji bangi,ugoro,sigara,cocaine, mirungi, kubeli n.k
- iii) Kupiga au kupigana.
- iv) Ubakaji , kufanya ngono , kuoia au kuolewa , kubeba au kusababisha mimba, usagaji na ushoga.
- v) Kutoa mimba
- vi) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- vii) Kukataa adhabu kwa makusudi na kutoa lugha ya matusi
- viii) Uvivu , kukwepa kazi na kusema uongo
- ix) Kuwa na simu ya mkononi
- x) Kudharau bendera ya Taifa.
- xi) Kuwa na silaha shuleni au bwenini kama vile kisu, rungu, fimbo n.k
- xii) Kuwasha moto bwenini mfano; pasi ya mkaa na umeme, mshumaa,kibatari n.k
- xiii) Kukwepa masomo au kutofanya mitihani bila sababu maalumu
- xiv) Kutoroka shuleni na kuonekana kwenye miji ya watu na vibanda vya mpira bila sababu maalumu.
- xv) Kutumia madawa ya kubadili rangi ya ngozi, nywele au kucha.
- xvi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

4.0 HITIMISHO

4.1 Tafadhali soma kwa makini maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

4.2 Nakutakia maandalizi mema na karibu sana Parakuyo sekondari.

.....
LEIYO L. SEPUKE
MKUU WA SHULE
(0672678869/0753484701)

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrant to

.....

Full Name:

1. Aids Test:
2. Blood Count (Red & White):
3. Stool Examination:
4. Urine Examination:
5. Syphilis Test:
6. T.B. Test:
7. Eye Test:
8. Ear Test:
9. Spleen:
10. Abdomen:
11. Additional information or any other physical, mental hereditary or infections diseases:
.....
.....

12. Treatment after Examination:-
.....
.....

(Please state nature of treatment)

Medical Certificate

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to per sue further education.

Signature:

Renintation:

Station:

Official Stamp*

HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA.

SHULE YA SEKONDARI PARAKUYO,

S.L.P 65,

KIMAMBA-KILOSA.

TAREHE.....

HATI YA UTII WA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.

Mimi

Mtoto wa Bwana/Bibi.....

Mbele ya Baba/ Mama/Mlezi.....

Nakiri kwamba nimesoma na kuelewa kwa makini sheria na kanuni za shule kama zilivyoandikwa katika barua ya kujiunga na shule ya sekondari Parakuyo ya tarehe.....

Ninazikubali sheria na kanuni hizo, nitazifuata na kutii nikijua kuwa ninaelimishwa na umma kwa manufaa yangu mimi na manufaa ya umma.

Sahihi ya mwanafunzi.....

Tarehe

Mimi Bwana/ Bibi

Mzazi / Mlezi wa

Nakiri kwamba nimesoma na kuelewa kwa makini sheria na kanuni za shule kama zilivyoandikwa katika barua ya kujiunga shule ya sekondari Parakuyo ya tarehe

Ninazikubali sheria na kanuni hizo na ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kuona kuwa mwanangu..... anazifuata kwa manufaa yake na manufaa ya umma. Aidha naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika kutekeleza maelekezo yote yatakayotolewa na shule.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi

Tarehe